JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**



# MWONGOZO WA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA DAWATI LA KUTOKOMEZA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA KATIKA MAENEO YA UMMA

**JANUARI, 2023**

**WIZARA YA MJJWMM**
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
@wizarayamaendeleojamiiz www.jamii.go.tz jamii online Tv

Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya
S. L. P 573, 40478 DODOMA
Barua pepe:ps@jamii.go.tz
Tovuti: WWW.jamii.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# MWONGOZO WA UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA DAWATI LA KUTOKOMEZA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA KATIKA MAENEO YA UMMA

**JANUARI, 2023**

# YALIYOMO

VIFUPISHO………………………………………………………….…….iv

ISTILAHI…………………………..………………………………….....vi

DIBAJI…………………………………………………………………..ix

SEHEMU YA KWANZA…………………………………………….....1

1.0 UTANGULIZI…………………………….……………………….1

1.1 CHIMBUKO LA MWONGOZO……………………………......2

1.2 MISINGI YA KISHERIA…………………………………..….3

1.3 MALENGO YA MWONGOZO………………………………4

1.3.1 LENGO KUU………………………………..………………4

1.3.2 MALENGO MAHUSUSI…………………………………...4

1.4 UMUHIMU WA MWONGOZO……………………………...5

1.5 WALENGWA WA MWONGOZO…………………………..….5

SEHEMU YA PILI……………………………………………...……..6

2.0 UANZISHWAJI WA DAWATI LA KUTOKOMEZA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA KATIKA MAENEO YA UMMA……………………………………………………………………6

2.1 UANZISHAJI WA DAWATI…………………………………..6

2.2 MAJUKUMU YA DAWATI……………………………..……....6

2.3 MUUNDO WA DAWATI…………………………………………7

2.4 SIFA ZA WAJUMBE WA DAWATI………………………......8

2.5 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA DAWATI……………..…....9

2.6 MUDA WA UONGOZI WA DAWATI……………………......10

SEHEMU YA TATU……………………………….……………11
3.0 UENDESHAJI WA DAWATI LA KUTOKOMEZA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA KATIKA MAENEO YA UMMA…..........................................................................11
3.1 UWASILISHAJI WA TAARIFA……………………….....…11
3.2 VIKAO VYA DAWATI……………………………….....….12
3.2.1 VIKAO VYA ROBO…………………………………………….12
3.2.2 VIKAO VYA DHARURA………………………….....…….13
3.3 UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO KATIKA DAWATI…………………………………………………..13
3.3.1 KUPOKEA TAARIFA ZA MALALAMIKO NA NAMNA YA KUSHUGHULIKIA…………………………………………………13
3.3.1.1 ELIMU KUHUSIANA NA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA……………………………………………………………….14
3.3.2 HUDUMA KWA WAHANGA WA UKATILI………………..15
SEHEMU YA NNE……………………………………………….16
4.0 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU……...…………...16
4.1 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM…...…………………...….16
4.2 OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA……….………………………………………...………….17

4.3 MAJUKUMU YA WIZARA ZA KISEKTA NA IDARA ZINAZOJITEGEMEA ZA UMMA…………………………………….18

4.4 SEKTA BINAFSI NA WADAU WA MAENDELEO………..19

SEHEMU YA TANO……………………………………………..20

5.0 URATIBU, TATHIMINI NA UFUATILIAJI……………...…20

5.1 URATIBU…………………………………………………….20

5.2 UFUATILIAJI………...………………………………………20

5.3 TATHIMINI………………...………………………………22

SEHEMU YA SITA…………………………………………….....23

6.0 HITIMISHO……………………………………………………..23

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACRWC** | Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (African Charter on Rights and Welfare of the Child) |
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **CEDAW** | Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (Convention for Elimination of All Forms of Discrimination Against Women) |
| **CPA** | Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Criminal Procedure Act) |
| **CRC** | Mkataba wa Haki za Mtoto (Convention on the rights of the Child) |
| **EfG** | Equality for Growth |
| **MTAKUWWA** | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18-2021/22) |
| **OR- TAMISEMI** | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **WEO** | Afisa Mtendaji wa Kata (Ward Executive Officer) |

| | |
|---|---|
| **AFUA** | Shughuli Mbalimbali zinazotekelezwa katika jamii kwa maendeleo ya Taifa |
| **LHR** | Legal and Human Rights |

## ISTILAHI

| | | |
|---|---|---|
| 1 | **Dawati la kutokomeza Ukatili wa Kijinsia** | Ni Jukwaa maalum linaloundwa katika eneo la Umma mahsus kwa ajili ya kushughulikia na kuimarisha mfumo wa kutokomeza Ukatili wa Kijinsia Maeneo hayo ni kama vile Sokoni, Kambi/Vituo vya michezo, Maeneo ya Fukwe, Viwanja vya Ndege, Bandarini, Stesheni za Gari Moshi, Vituo vya Bodaboda, Bajaji na Taxi, Vituo vya Daladala/Mabasi, Mialo/Bandari za Uvuvi, Kambi za Uvuvi, Migodini, Kambi za waathirika wa Maafa na Minada/Magulio yaliyoundwa |
| 2 | **Jinsi** | Ni hali ya kibaolojia inayombainisha mtu kuwa wa kike au wa kiume |
| 3 | **Jinsia** | Ni dhana inayoonyesha mahusiano yanayojengwa na jamii ili kutofautisha kati ya wanaume na wanawake ambapo mahusiano hayo yanagawa majukumu na haki tofauti kwa kila jinsi kutegemeana na utamaduni, mila na desturi. |
| 4 | **Maeneo ya Umma** | Ni sehemu yoyote ya wazi inayoweza kupatikana kwenye maeneo ya Serikali au ya Taasisi Binafsi kama vile ya Sokoni, |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kambi/vituo vya michezo, Maeneo ya fukwe, Viwanja vya Ndege, Bandarini, Stesheni za Gari Moshi, Vituo vya Bodaboda, Bajaji na Taxi, Vituo vya Daladala/Mabasi, Mialo/Bandari za Uvuvi, Kambi za Uvuvi, Migodini, Kambi za waathirika wa Maafa na Minada/Magulioni ambapo watu hukusanyika kwa ajili ya huduma za kibinadamu, kijamii na kiuchumi |
| 5 | **Kamati** | Ni uongozi uliochaguliwa au kuteuliwa kwa ajili ya uratibu na usimamizi katika eneo husika. |
| 6 | **Uongozi** | Ni utawala uliopo kwenye eneo husika kwa ajili ya uratibu na usimamizi. |
| 7 | **Mhanga** | Ni mtu (wa kike au wa kiume) aliefanyiwa vitendo vya Ukatili wa Kijinsia. |
| 8 | **Ukatili wa Kijinsia** | Ni kitendo chochote chenye madhara anachofanyiwa mwanamke/mwanaume na kumuathiri kimwili, kiafya, kiuchumi, kiakili au kisaikolojia. |
| 9 | **Usawa wa Kijinsia** | Ni Uwepo wa haki na fursa sawa kwa jinsi zote kushirikishwa kwa usawa bila kujali kuwa ni mwanamke au mwanaume. |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | **Wadau** | Ni Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Umma, Taasisi Binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali ambazo Mwongozo huu unawagusa kwa njia moja au nyingine |

# DIBAJI

Ukatili wa Kijinsia una athari kubwa katika jamii ikiwemo majeraha, ulemavu, matatizo ya kisaikolojia na hata vifo kwa wanawake, wanaume, vijana wa kike na kiume. Athari hizo ni kikwazo cha maendeleo kwa makundi haya katika kushiriki shughuli za kiuchumi na kijamii. Kutokana na kuwepo kwa vitendo vya ukatili nchini, Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na vitendo vya ukatili nchini.

Jitihada hizo ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) na Mkakati wake wa Utekelezaji (2005); Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); Sheria ya Mtoto sura ya 13 na Kanuni zake na Sheria ya Ushahidi Sura ya 16. Vilevile kuanzishwa kwa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22) na Kampeni mbalimbali za kupinga Ukatili wa Kijinsia ikiwemo ya **‘‘Twende Pamoja Ukatili wa Kijinsia Tanzania Sasa Basi’’**

Matokeo ya Tathmini ya MTAKUWWA ya Mwaka 2022, imeonesha kuwa Ukatili wa Kijinsia umeenea kote nchini na kushamiri huko kunachangiwa na uwepo wa ndoa za utotoni, uchumi tegemezi kwa jamii kubwa, ukosefu wa miundombinu bora, mila na desturi zenye madhara kwa jamii, hali duni ya maisha pamoja na kiwango kidogo cha elimu. Aidha, utafiti wa haki za binadamu umebainisha kuwa asilimia 52% ya wahojiwa waliona unyanyasaji dhidi ya wanawake ni tatizo kubwa la ukatili katika jamii licha ya uwepo wa matukio mengi

ya Ukatili wa Kijinsia kwa wanaume na wazee. Unyanyasaji wa kimwili, Ukatili wa Kijinsia kwa njia ya ubakaji na kulawiti, unyanyasaji wa kisaikolojia na rushwa ya ngono ni miongoni mwa vitendo vya ukatili ambavyo wanawake na wasichana wanakabiliana nao.

Serikali kwa kushirikiana na Wadau inahitaji kuchukua hatua za haraka zaidi kwa ajili ya kulinda kundi hili linaloathirika na vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto.

Aidha, Serikali kwa kutambua hilo imeandaa Mwongozo wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Dawati la Kutokomeza Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo ya Umma, ambao umelenga kuweka muundo na utaratibu wa kuratibu uanzishwaji, uendeshaji na ufuatiliaji wa dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma. Maeneo hayo ya umma ni pamoja na Sokoni, Kambi/Vituo vya Michezo, Maeneo ya Fukwe, Viwanja vya Ndege, Bandarini, Stesheni za Gari Moshi, Vituo vya Bodaboda, Bajaji na Taxi, Vituo vya Daladala/Mabasi, Mialo/Bandari za Uvuvi, Kambi za Uvuvi, Migodini, Kambi za waathirika wa Maafa na Minada/Magulio.

Ni matumaini yangu kuwa wadau wote wakiwemo Wizara za Kisekta, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati za Uongozi zinazosimamia maeneo ya umma, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi, Makampuni na Wadau kwa ujamla watatumia Mwongozo huu kama nyenzo elekezi katika

kutekeleza masuala yote ya kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma nchini.

**DKT. ZAINAB A.S CHAULA**
**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na vitendo vya ukatili nchini. Aidha, Serikali kupitia iliyokuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na sasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeendelea kusimamia afua za kimkakati zilizojumuishwa katika Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22).

Pamoja na jitihada hizo vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeendelea kuwepo katika maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya umma. Tathmini ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18- 2021/22), imeonesha kuwa ukatili wa kijinsia umeenea kote nchini na miongoni mwa sababu kwa mujibu wa utafiti huo ni pamoja na ndoa za utotoni, uchumi tegemezi kwa jamii kubwa na kiwango kidogo cha elimu (Benki ya Dunia). Vilevile, kwa mujibu wa ripoti ya Haki za Binadamu ''*Legal Human Right''* (LHR,2021) imebainisha unyanyasaji wa kimwili, ukatili wa kijinsia kwa njia ya ubakaji na kulawiti, unyanyasaji wa kisaikolojia na rushwa ya ngono kuwa ni aina za ukatili ambazo wanawake na wasichana walikabiliana nazo. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa, takriban nusu ya waliohojiwa katika utafiti wa Haki za Binadamu (asilimia 52) waliona unyanyasaji dhidi ya wanawake kama tatizo kubwa katika jamii yao. Hata hivyo, kumekuwa na matukio mengi ya ukatili wa kijinsia kwa wanaume na wazee.

## 1.1 CHIMBUKO LA MWONGOZO

Chimbuko la Mwongozo huu ni pamoja na tathimini ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22) ambapo tathimini yake ilionesha kuwa bado kuna vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa Wanawake, Watoto, Wanaume na Wazee ambavyo vinaendelea kutokea katika jamii.

Matokeo ya Utafiti wa Mwaka 2017 na 2019, uliofanywa na Shirika la *Equality for Growth* (EfG) kuhusu ukatili wa kijinsia kwenye masoko na kuhusisha Mikoa minne (4) ya Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga na Dodoma, umebaini uwepo wa matukio ya ukatili wa kijinsia sokoni. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam asilimia 39.7 kati ya watu 124 walibainika kufanyiwa ukatili wa unyanyasaji na shambulio la aibu, ambapo asilimia 32 walifanyiwa ukatili wa kisaikolojia, Asilimia 24.3 walifanyiwa ukatili wa kingono na silimia 4% ni ukatili wa kimwili. Aidha, Mkoa wa Shinyanga tafiti ilionesha kuwa, ukatili wa kiuchumi ni asilimia 34 kwa watu 68 waliofanyiwa ukatili. Kati yao asilimia 31 walifanyiwa ukatili wa kisaikolojia, asilimia 28 ukatili wa kimwili, asilimia 4 ukatili wa kingono na asilimia 4 walifanyiwa aina nyingine za ukatili. Mkoa wa Dodoma utafiti umeonesha kuwa asilimia 32 ya watu 60 walifanyiwa ukatili wa shambulio la aibu, asilimia 31 ya watu 58 walifanyiwa ukatili wa kisaikolojia, asilimia 21 ukatili wa kiuchumi, asilimia 8 ukatili wa kimwili na aina nyinginezo ilikuwa asilimia 8. Mkoa wa Mwanza ilionesha kuwa asilimia 50 ya watu walifanyiwa ukatili wa kiuchumi, ikijumuisha asilimia 25 walifaniwa ukatili wa kisaikolojia, asilimia 20 walifanyiwa ukatili wa kimwili na asilimia 5 walifanyiwa aina nyingine za ukatili. (EfG 2017-2019).

Kwa kuzingatia matokeo ya tafiti hizo ni dhahiri kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia hususan katika maeneo ya umma bado

vipo, hivyo kupelekea kuandaliwa kwa Mwongozo huu ambao utaongeza kasi ya juhudi za kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

## 1.2 MISINGI YA KISHERIA

Uandaaji wa Mwongozo huu umezingatia misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sera, Ilani ya Chama Tawala ya mwaka 2020-2025, Sheria, Mipango, Mikakati na maelekezo ya Serikali kama ifuatavyo.

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Sehemu ya tatu ibara ya 12 na 13;
(ii) Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 na Mkakati wa utekelezaji wake wa mwaka 2005;
(iii) Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008;
(iv) Sheria ya Ushahidi Sura ya 16;
(v) Sheria ya Kutokomeza na Kupambana na Rushwa Sura ya 329;
(vi) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20;
(vii) Sheria ya Mtoto sura ya 13;
(viii) Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18-2022/22;
(ix) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu wa mwaka 2017-2022;
(x) Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025 ibara ya 231 (a), (i), na (i)
(xi) Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikihusisha: Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa

aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake-CEDAW (1979); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (1989); Malengo ya Maendeleo Endelevu- SDGs (2015); Ajenda ya Maendeleo ya Afrika Tuitakayo (2063); Mkataba wa Haki za Mtoto - CRC (1989); Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto - ACRWC (1990);

(xii) Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025); na

(xiii) Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano III (2021/22 – 2025/26).

## 1.3 MALENGO YA MWONGOZO

### 1.3.1 LENGO KUU

Kuweka muundo na utaratibu wa kuanzisha, kuendesha na kufuatilia dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma.

### 1.3.2 MALENGO MAHUSUSI

Malengo mahsusi ya Mwongozo huu ni;

i. Kuanzisha Dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia; katika maeneo ya umma;
ii. Kuwajengea uwezo Viongozi/Kamati zilizopo katika kushughulikia mashauri ya vitendo vya ukatili katika maeneo ya umma.
iii. Kuweka utaratibu unaofaa wa kutoa taarifa na kushughulikia mashauri ya vitendo vya ukatili katika maeneo ya umma;

## 1.4 UMUHIMU WA MWONGOZO

Serikali inaheshimu misingi ya Utu na Haki za Binadamu. Hivyo, Mwongozo wa kupinga ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma ni wa muhimu na utawezesha: -

(i) Uanzishwaji, uendeshaji na ufuatiliaji wa Dawati la jinsia kwenye maeneo ya umma;
(ii) Kuimarisha juhudi za kutokomeza Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo ya umma;
(iii) Kutoa mwongozo na maelekezo kuhusu muundo wa uanzishwaji na uendeshaji wa Dawati katika meneo ya umma;
(iv) Kuzingatia masuala ya jinsia katika maeneo ya umma; na
(v) Kujenga uelewa wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma.

## 1.5 WALENGWA WA MWONGOZO

Mwongozo huu ni kwa ajili ya maeneo ya umma na umelenga kutumiwa na wadau wote wenye shughuli kwenye maeneo ya umma au kuguswa na utekelezaji wa maeneo ya umma. Wadau hao ni pamoja na wananchi wenye shughuli kwenye maeneo hayo ya umma, Wizara za Kisekta, Idara za Serikali Zinazojitegemea, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati za Uongozi zinazosimamia maeneo ya umma, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi Binafsi na Makampuni.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UANZISHWAJI WA DAWATI LA KUTOKOMEZA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA KATIKA MAENEO YA UMMA

Sehemu hii inaeleza muundo na majukumu ya Dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma. Viongozi wa dawati watatekeleza majukumu yao kwa kushirikiana na Uongozi unaosimamia eneo/kituo husika kulingana na Sheria, Taratibu na Miongozo inayosimamia na kuongoza sehemu hiyo

### 2.1 UANZISHAJI WA DAWATI

Kila eneo la umma linapaswa kuanzisha Dawati mahsusi la kutokomeza vitendo vya ukatili ambalo majukumu yake itakuwa kusimamia, kufuatilia na kushughulikia vitendo vya ukatili kwenye eneo hilo. Aidha, Dawati litakuwa na majukumu mahsusi na kuzingatia muundo uliowekwa. Majukumu ya Dawati, Sifa na Muundo wa Uongozi ni ifuatavyo: -

### 2.2 MAJUKUMU YA DAWATI

Katika kuhakikisha kuwa maeneo ya umma yanakuwa rafiki na salama kwa jamii dawati litakuwa na majukumu yafuatayo;

(i) Kuandaa Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mwaka ambao utaidhinishwa na Uongozi wa eneo husika lenye dawati

(ii) Kutoa elimu inayohusu afua za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia;

(iii) Kushirikiana na Uongozi/Kamati wa eneo husika katika kusimamia kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia;

(iv) Kutoa huduma kwa Wahanga wa Ukatili na kutoa rufaa;

(v) Kupokea taarifa za ukatili wa kijinsia na kuzishughulikia;

(vi) Kutunza kumbukumbu za ukatili wa kijinsia maeneo ya umma;

(vii) Kuandaa taarifa ya utendaji na uendeshaji wa dawati ya robo mwaka na kuiwasilisha ngazi husika baada ya kuidhinishwa na Uongozi wa eneo husika;

(viii) Kushirikiana na Uongozi /Kamati inayosimamia eneo husika kuandaa kanuni/taratibu zitakazoongoza maeneo ya umma kuhusiana na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia; na

(ix) Kuhamasisha jamii kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia.

## 2.3 MUUNDO WA DAWATI

Dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili katika maeneo ya umma litakuwa na wajumbe kumi (10) ambao ni

(i) Afisa Maendeleo ya Jamii katika eneo husika;

(ii) Afisa Ustawi wa Jamii;

(iii) Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa au mjumbe atakayemteua kumwakilisha kwenye Dawati hususan kwa kijiji/mtaa wenye maeneo zaidi ya moja ya umma;

(iv) Polisi Kata kutoka katika eneo husika na penye taasisi nyingi zenye madawati anaweza kutuma mwakilishi; na

(v) Tabibu/Mganga kutoka kituo cha huduma za afya kilichopo eneo husika na penye taasisi nyingi zenye Ma-dawati eneo hilo anaweza kutuma mwakilishi wake,

(vi) Mtaalamu ambaye ni msimamizi wake eneo husika la umma;

(vii) Wajumbe wengine wanne (4) watateuliwa kutoka eneo husika.

Aidha, wajumbe ambao wametajwa kwa nyadhifa zao wataingia moja kwa moja kwenye Kamati. Wajumbe waliobaki watateuliwa kupitia Uongozi wa sehemu husika na uwiano (jinsi) unapaswa kuzingatiwa.

**Zingatia:**

(i) Mjumbe ambaye ni mtaalam kama alivyoainishwa romani (vi) anapaswa atokane na huduma inayotolewa katika eneo husika. Mfano endapo Dawati ni eneo la stendi ya magari, sharti mjumbe mmojawapo atoke Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA)

(ii) Wajumbe wa Dawati watachagua Mwenyekiti na Katibu kutoka miongoni mwao.

## 2.4 SIFA ZA WAJUMBE WA DAWATI

Mjumbe wa Dawati anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo;

(i) Awe ni raia wa Tanzania;

(ii) Awe na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea;

(iii) Awe mwenye akili timamu;
(iv) Awe ni mtu anayekubalika katika jamii;
(v) Awe hakuwahi kutiwa hatiani katika mahakama yoyote kwa kosa lolote la jinai;
(vi) Awe na uwezo wa kusimamia haki kwa usawa na uadilifu; na
(vii) Awe mwadilifu

## 2.5 MAJUKUMU YA VIONGOZI WA DAWATI

### 2.5.1 MAJUKUMU YA MWENYEKITI

(i) Kuwasilisha Mpango Kazi wa Mwaka wa Utekelezaji wa Dawati ulioidhinishwa na Uongozi wa eneo husika
(ii) Kutoa elimu inayohusu afua za kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia;
(iii) Kushirikiana na Uongozi wa eneo husika katika kusimamia kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia;
(iv) Kusimamia uendeshaji wa Dawati;
(v) Kuitisha na kuendesha vikao vya Dawati na
(vi) Kushirikiana na Uongozi/Kamati kuandaa Kanuni/Taratibu zitakazoongoza maeneo ya umma kuhusiana na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia.

### 2.5.2 MAJUKUMU YA KATIBU WA DAWATI

(i) Kuratibu uandaaji wa Mpango kazi wa mwaka wa utekelezaji wa shughuli za kamati na

kuuwasilisha kwa uongozi wa eneo husika la umma kwa ajili ya kuidhinishwa

(ii) Kuratibu utoaji elimu kwa umma kwa rasilimali zilizopo na kwa kushirikiana na wadau kuhusu ukatili wa kijinsia katika eneo lake husika;
(iii) Kupokea na kusajili matukio ya Ukatili wa Kijinsia kwa kutumia fomu maalum;
(iv) Kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika na tukio hilo;
(v) Kutunza kumbukumbu za vitendo vya ukatili wa kijinsia maeneo ya umma;
(vi) Kujenga mahusiano na ushirikiano kati ya Dawati na Uongozi wa eneo husika;
(vii) Kuandaa muhtasari wa kikao; na
(viii) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Dawati.

## 2.6 MUDA WA UONGOZI WA DAWATI

Uongozi na Wajumbe wa Dawati watadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja. Uongozi wa eneo husika utapaswa kusimamia uteuzi wa Wajumbe na Viongozi wa Dawati kila baada ya muda huo.

**Zingatia:**

Uratibu wa Dawati hili utakuwa chini ya Mamlaka inayosimamia eneo husika kama vile Uongozi wa Soko, Uongozi wa maeneo ya Usafiri, Uongozi wa maeneo ya Fukwe na Uongozi wa maeneo ya Michezo. Dawati litazingatia Uwiano ulio sawa (jinsi) kwenye Uongozi, nafasi za maamuzi pamoja na kundi la Watu Wenye Mahitaji Maalum.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UENDESHAJI WA DAWATI LA KUTOKOMEZA VITENDO VYA UKATILI WA JINSIA KATIKA MAENEO YA UMMA

Uendeshaji wa Dawati utahusisha utekelezaji wa majukumu ya Dawati pamoja na utaratibu wa uendeshaji wa vikao. Dawati litashirikiana na Uongozi wa Kamati ya eneo husika pamoja na Ma-dawati mengine ya kuzuia vitendo vya ukatili katika maeneo ya umma kutoa elimu na huduma kwa wahanga wa ukatili pamoja na rufaa. Pia, Dawati litatunza kumbukumbu za vitendo vya ukatili vilivyoripotiwa na kushughulikiwa.

### 3.1 UWASILISHAJI WA TAARIFA

Viongozi wa Dawati watawasilisha kwa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji wa eneo husika taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Dawati ambayo imeidhinishwa na Uongozi wa eneo husika la umma. Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji ambaye ni Mratibu wa MTAKUWWA ngazi hiyo ataunganisha taarifa hiyo kwenye ajenda za Kamati ya MTAKUWWA ili nao wafahamu yanayojiri kwenye eneo lao kwa dhamana yao na kushirikiana kwenye mipango ya kudhibiti. Vilevile, Mtendaji wa Mtaa/Kijiji atawasilisha taarifa hiyo kwa Mtendaji wa Kata ili aunganishe na za maeneo mengine ya vituo vya Kata hiyo na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye ni Mwenyekiti wa MTAKUWWA ngazi ya Halmashauri. Nakala za taarifa hizo atapewa Afisa Maendeleo ya Jamii/Afisa Ustawi wa jamii wa Kata kwa hatua zao kitaalamu na kwa wakati.

Ikumbukwe, itifaki yote ya uwasilishaji taarifa za Serikali inatakiwa kuzingatiwa ili ajenda hii iwe ya kudumu kwenye vikao vyote vya Serikali vya kisheria kuanzia Mikutano ya Kijiji, Halmashauri ya Kijiji, Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC), Menejimenti ya Halmashauri, Kamati za Kudumu za Baraza la Madiwani hususan Kamati ya Huduma za Jamii, Utawala, Mipango na Fedha na hatimaye Baraza la Madiwani. Vikao vingine ni kwenye Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC), Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na Kamati za MTAKUWWA ngazi zote. Majumuisho kutoka ngazi ya Mkoa yatawasilishwa Wizarani kupitia Wizara ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na nakala Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa hatua zake za kisera na uratibu kupitia Kamati Tendaji ya MTAKUWWA.

Ni kwa kufanya hivi ndiyo ajenda hii itamilikiwa na wananchi, wawakilishi wa wananchi na viongozi na wadau ngazi zote na kuleta msukumo wa pamoja kwenye kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia na kwa watoto na makundi mengine yaliyotajwa kwenye Mwongozo huu.

## 3.2 VIKAO VYA DAWATI

Dawati litakuwa na vikao vine (4) kwa mwaka, vitakavyofanyika mara moja kila baada ya miezi mitatu (3) ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya Dawati. Aidha, vikao vya dharura vitafanyika wakati wowote kutokana na uhitaji.

### 3.2.1 VIKAO VYA ROBO

(i) Vikao hivi vitajadili taarifa ya utekelezaji wa kamati ya kila robo mwaka

(ii) Vikao hivi vitafanyika wiki ya pili ya robo mwaka;

(iii) Wajumbe watajulishwa tarehe ya kikao siku 7 kabla ya kikao husika ikiambatana na agenda;
(iv) Akidi ya kikao itakuwa ni nusu ya wajumbe;
(v) Pamoja na agenda zingine kikao cha robo mwaka kitajadili taarifa za matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia na hatua zilizochukuliwa;
(vi) Muhtasari wa taarifa ya kikao utawasilishwa kwa Uongozi/Kamati ya eneo husika kabla ya kuwasilishwa kwa Viongozi wa Kitongoji/Kijiji, Kata na Mamlaka za Serikali ya Mitaa na kufuata utaratibu kama ilivyoelezwa hapo awali kwenye 3.1.
(vii) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya dharura.

### 3.2.2 VIKAO VYA DHARURA

(i) Kutakuwa na Vikao vya dharura endapo itahitajika kufanyika kutokana na dharura iliyojitokeza na kuhitaji kushughulikiwa kwa haraka; aidha, ni vema kujitahidi kupunguza dharura kwa kuweka mipango na mifumo thabiti na ikiwezekana visizidi idadi ya vikao vya kawaida.

## 3.3 UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO KATIKA DAWATI

### 3.3.1 KUPOKEA TAARIFA ZA MALALAMIKO NA NAMNA YA KUSHUGHULIKIA

(i) Taarifa za malalamiko ya vitendo vya ukatili zitawasilishwa kwenye Dawati na mtu yeyote

au wahanga wa vitendo vya ukatili wenye taarifa kuhusu ukatili au viashiria vya ukatili;

(ii) Taarifa za ukatili zitaingizwa katika fomu ambayo ni Regista ya vitendo vya ukatili wa kijinsia;

(iii) Taarifa za malalamiko zenye kuhitaji huduma za rufaa zitawasilishwa katika Taasisi husika kama vile, Ofisi ya Ustawi wa Jamii, Nyumba Salama, Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi kwa ajili ya hatua za kisheria; na

(iv) Muhanga au mtoa taarifa wa vitendo vya ukatili atapaswa kutoa taarifa kwenye Dawati kuhusu viashiria vyovyote vinavyohusiana na vitisho au vikwazo atakavyowekewa na mtuhumiwa, marafiki au ndugu wa mtuhumiwa.

### 3.3.1.1 ELIMU KUHUSIANA NA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA

(i) Dawati kwa kushirikiana na Uongozi/Kamati katika eneo husika litaandaa matangazo kwa kutumia njia mbalimbali kama vile mabango, vipeperushi, vipaza sauti yenye ujumbe wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo umma;

(ii) Kuhamasisha kwa njia ya mikutano, katika maeneo ya umma;

(iii) Kutoa elimu kupitia mitandao ya kijamii na redio za kijamii; na

(iv) Kutumia watu wenye ushawishi, (wasanii, wazee maarufu, na viongozi wa dini) kwa ajili ya kuelimisha kuhusu kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma

(v) Kutoa elimu kwa mtu mmoja mmoja atakayefika kwenye Dawati; na
(vi) Kutoa elimu kupitia makongamano mbalimbali kwa ajili ya kuelimisha Jamii;

### 3.3.2 HUDUMA KWA WAHANGA WA UKATILI

Dawati wakati wa kutoa huduma kwa Wahanga wa Ukatili litazingatia mambo yafuatayo:

Mhanga wa Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia anapaswa kusikilizwa bila kuwa na mtazamo hasi kwa tukio lililomtokea na kupewa rufaa;

(i) Kupewa faragha na usiri;
(ii) Kulindwa dhidi ya vitisho; na
(iii) Kupewa nafasi ya kutoa maoni na kusikilizwa bila upendeleo na ubaguzi.

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU

Majukumu ya Wadau muhimu wanaohusika na uratibu, usimamizi na uendeshaji wa Dawati kwenye maeneo ya umma yameainishwa ili kutoa urahisi wa utekelezaji. Wadau hao ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, OR TAMISEMI, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

## 4.1 WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM.

Wizara hii itakuwa na majukumu yafutayo:

(i) Kutoa maelekezo ya kisera, kisheria miongozo na kanuni kuhusu Kupinga ukatili wa Kijinsia.

(ii) Kuandaa miongozo ya kufundishia kuhusu kupinga ukatili wa Kijinsia maeneo ya Umma

(iii) Kuratibu utoaji wa mafunzo kwa watalaam wa kisekta katika ngazi ya Kitaifa, Mikoa na Serikali za mitaa kuhusu Kupinga ukatili wa Kijinsia katika maeneo ya umma;

(iv) Kufanya tathimini na kutoa taarifa na mrejesho kwa wadau kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Dawati la Kupinga ukatili wa Kijinsia katika maeneo ya umma

## 4.2 OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

Wizara hii itakuwa na majukumu yafutayo:

(i) Kuratibu utekelezaji wa afua za kuzuia ukatili kwenye maeneo ya umma kwenye mamlaka chini ya wizara hii,

(ii) Kuratibu upatikanaji wa taarifa na kuhakikisha taarifa hizo ni sehemu zinazojumuishwa kwenye taarifa inayowasilishwa kwenye vikao vya kisheria vya kila ngazi kama ilivyoanishwa kwenye 3.1 hapo awali.

(iii) Kuhakikisha maeneo yote ya umma yanaanzisha Dawati la kuzuia ukatili wa kijinsia katika maeneo yao kulingana na Mwongozo.

(iv) Kuratibu na kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa Dawati la Kupinga Ukatili wa Kijinsia katika maeneo ya umma kwa kushirikiana na Wizara za kisekta.

(v) Kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa mashauri ya matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyowasilishwa kwenye vyombo mbalimbali vya kisheria.

(vi) Kuratibu upatikanaji wa taarifa za robo mwaka kuhusu dawati kutoka Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa; na

(vii) Kuratibu Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa majukumu yote ya Dawati la kuzuia ukatili wa Kijinsia kwenye maeneo ya Umma kwa kushirikiana na wataalamu wa wizara za kisekta.

## 4.3 MAJUKUMU YA WIZARA ZA KISEKTA NA IDARA ZINAZOJITEGEMEA ZA UMMA

Wizara za Kisekta na Idara zinazojitegemea za umma zinazoguswa na utekelezaji wa Mwongozo huu ni pamoja na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Maliasili na Utalii. Wizara hizi zitakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuhakikisha Dawati la kuzuia vitendo vya ukatili linaanzishwa /kuanzishwa kwa kuzingatia Mwongozo huu;
(ii) Kusimamia haki za wahanga wa vitendo vya ukatili wa kijinsia maeneo ya umma (Jeshi la Polisi, Mahakama na TAKUKURU;
(iii) Kutoa huduma stahiki za afya na unasihi kwa wahanga wa vitendo vya ukatili wa kijinsia maeneo ya umma (Tiba na Afya)
(iv) Kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kufanya tathimini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo wa kuzuia vitendo vya ukatili maeneo ya umma; na
(v) Kuandaa na kutoa taarifa ya jumla ya utekelezaji wa Mwongozo wa kuzuia vitendo vya ukatili kwenye maeneo ya umma kupitia mifumo rasmi ya utendaji

## 4.4 SEKTA BINAFSI NA WADAU WA MAENDELEO

Sekta binafsi hususan Asasi za Kiraia (AZAKI), Mashirika Binafsi Makampuni, Taasisi za kimataifa na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa watakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kushirikiana na Serikali katika kuzuia vitendo vya ukatili maeneo ya umma.

(ii) Kuwezesha upatikanaji wa rasimali za utekelezaji wa afua za kuzuia vitendo vya ukatili kwenye maeneo ya umma.

(iii) Kushirikiana na Uongozi wa Dawati kutoa elimu na msaada wa kisheria na ushauri wa kitaaluma kwa wahanga

(iv) Kuyajengea uwezo Madawati ya kuzuia ukatili katika maeneo ya umma.

(v) Kushirikiana na Serikali katika kufanya ufuatiliaji, tathmini na usimamizi saidizi kwa Madawati.

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 URATIBU, TATHMINI NA UFUATILIAJI

### 5.1 URATIBU

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika kuhakikisha ufanisi wa Dawati, itatekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuratibu wadau wa kisekta waweze kuona kipaumbele kwenye kufanikisha uanzishwaji wa Madawati ya kuzuia ukatili kwenye Maeneo ya Umma;

(ii) Kuratibu na kuwajengea uwezo Wajumbe wa Dawati la kuzuia vitendo vya Ukatili katika maeneo ya umma;

(iii) Kuratibu wadau wanaotekeleza uanzishaji wa Dawati la kuzuia ukatili wa kijinsia kwenye maeneo ya umma;

(iv) Kuratibu ufuatiliaji wa utendaji kazi wa Dawati la kuzuia ukatili maeneo ya umma;

(v) Kuratibu wadau kufanya tathmini ya utendaji wa Dawati la kuzuia vitendo vya ukatili katika maeneo ya umma; na

(vi) Kuratibu uchambuzi wa taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka zilizopokelewa kutoka OR-TAMISEMI, Wizara na Idara za kisekta zinazotekeleza Mwongozo huu.

### 5.2 UFUATILIAJI

Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo huu katika maeneo ya umma kila

robo mwaka ambapo upimaji wa utekelezaji utazingatia vipengele vifuatavyo: -

(i) Utengaji wa Fedha kwenye Bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya Dawati la kuzuia ukatili ndani ya Taasisi;
(ii) Utoaji mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Dawati;
(iii) Uwepo wa Takwimu za matukio yaliyoripotiwa kwenye Dawati la jinsia kwa uwiano wa wanawake na wanaume;
(iv) Uwepo wa mifumo ya utoaji wa taarifa mbalimbali za vitendo vya ukatili wa kijinsia kama vile simu, mifumo ya kielektroniki (dash board) na sanduku la kutolea maoni;
(v) Utekelezaji wa itifaki ya utoaji wa taarifa kama ilivyoelezwa kwenye kipengele na. 3.1 hapo juu.

Ikumbukwe kwamba ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo huu utaenda sambamba na viashiria vya matokeo vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Kutokomeza vitendo vya Ukatili kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na Mikakati mingine ya Kitaifa. Aidha, Taarifa za ufuatiliaji katika kila robo ya mwaka katika maeneo ya umma zitawasilishwa kwenye uongozi wa eneo husika, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara za Kisekta pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake Makundi Maalumu na baadae Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo, ndiyo inaratibu Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Ufuatiliaji utafanyika kwa kuzingatia viashiria vya utekelezaji vilivyowekwa katika mpangokazi huo wa MTAKUWWA.

## 5.3 TATHMINI

Utekelezaji wa shughuli za Dawati la Jinsia katika maeneo ya umma utafanyiwa tathmini kwa kipindi cha Mwaka mmoja ili kupima uingizwaji wa masuala ya jinsia na matokeo ya ushughulikiwaji wa vitendo vya ukatili kwenye maeneo ya umma katika ngazi husika. Aidha, Tathimini itahusisha kutumia viashiria vilivyowekwa katika mpangokazi kupitia shabaha na shughuli zitakazoainishwa kwa ajili ya utekelezaji. Tathmini itafanyika kwa kuhusisha na kushirikiana na Wadau kwa kila hatua na italenga kupima mchakato wa utekelezaji ili kuona matokeo na ufanisi na kuweza kubaini kama malengo tarajiwa yamefikiwa, hivyo kuwezesha wasimamizi na watekelezaji kufanya maamuzi stahiki ya maboresho kuhusu kushughulikia ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 HITIMISHO

Mwongozo huu ni nyenzo muhimu katika kuelekeza Wadau namna bora ya uanzishwaji, uratibu, uendeshaji na ufuatiliaji wa Dawati la kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma. Aidha, Mwongozo umeainisha muundo wa utendaji wa Dawati na majukumu yake ili kuweza kuimarisha ushughulikiaji wa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo yote ya umma.

Uwepo wa Mwongozo huu utasaidia kuimarisha afua za kutokomeza vitendo vya Ukatili wa Kijinsia katika Maeneo ya Umma. Vilevile utasaidia kujenga ushirikiano katika utendaji na uratibu baina ya wajumbe wa Dawati la kutokomeza ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma pamoja na Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia, Wizara za kisekta na Wadau wengine.

Hivyo, Mwongozo huu ni nyenzo na dira muhimu katika kuhakikisha kuwa aina zote za vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo ya umma vinatokomezwa ikiwa ni pamoja na uwekaji wa mazingira salama.

Katibu Mkuu
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya
S. L. P 573, 40478 DODOMA
Barua pepe:ps@jamii.go.tz
Tovuti: WWW.jamii.go.tz